



# MRADI WA EACOP

Mwaka 2006, mafuta ya kutoshereza kibiashara yaligundulika kuwepo katika bonde la Ziwa Albert nchini Uganda. Waen deshaji wa shughuli za mafuta nchini humo: CNOOC LTD, TOTAL na Tullow PLC wamekamilisha awamu ya uvumbuzi na sasa wanaelekea katika uendelezaji, ambao utaelekeza uzalishaji wa rasilmali hiyo ya mafuta nchini Uganda.

Mara baada ya kuzalishwa, sehemu ya mafuta ghafi itasafishwa nchini Uganda na kusambazwa kwenye soko la ndani na kiasi kingine kusafirishwa katika soko la kimataifa. Usafirishaji kwenda soko la kimataifa utatumia njia ya bomba la mafuta ghafi, litwalo "Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki" (The East Africa Crude Oil Export Pipeline - EACOP).

EACOP ni bomba la kusafirishia lenye urefu wa kilomita 1,445 ambalo litasafirisha mafuta ghafi ya Uganda kutoka Kabaale nchini humo hadi rasi ya Chongoleani iliyo karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania.

## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA JAMII (TAM) YA MRADI WA EACOP

Maana ya TAM ni Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Ni mchakato unaofafanua na kutathmini athari za mradi kwa mazingira na jamii na hatua za kukabiliana nazo. Uchunguzi huu wa TAM kuhusiana na mradi wa EACOP utafanyika katika njia ya bomba la usafirishaji mafuta ghafi (kutoka Kaabale nchini Uganda hadi mwambao wa Tanga, Tanzania) pamoja na kituo cha kuhifadhi mafuta (cha Chongoleani Tanga, Tanzania). Uchunguzi huu utafanyika kwa kuzingatia miongozo ya Kimataifa pamoja na Sheria za Serikali za Uganda na Tanzania.

## Mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii



### Awamu ya Uchunguzi waAwali

Kwanza huhusisha kuangalia eneo la mradi ili kubaini athari hasi na chanya zinazoweza kujitokeza na zikazohitaji utafiti wa kina.



### Tafiti za Wataalamu:

Awamu hii itahusisha tafiti mbalimbali. Kama sehemu ya uchunguzi huu, wataalamu kutoka nchini Uingereza (RSK), Uganda (ECO partners) na Tanzania (JSB na COWI) watatembelea baadhi ya vijiji vilivyo karibu na bomba, makambi pamoja na kituo cha kuhifadhi mafuta ili kuzungumza na wenyeji ili kupata uelewa juu ya hali ya maisha kwenye vijiji na mazingira ya asili.



### Awamu ya Tathmini ya Athari:

Katika awamu hii watafiti, wakisaidiwa na wenyeji wataainisha athari kwa maisha ya watu, mimea, wanyama, maji, hewa, udongo, manthari, utamaduni na afya zinazoweza kujitokeza kutokana na mradi wa EACOP juu ya.



### Kutengeneza Mipango wa Usimamizi:

Katika awamu hii ya mipango inatengenezwa ili kuepuka au kudhibiti athari hasi zitokanazo na mradi wa EACOP na pia kuongeza matokeo chanya.



### Uidhinishaji Kisheria:

Hatua hii ni ya uwasilishaji wa ripoti na uidhinishwaji na Serikali ya Uganda na Tanzania. Baada ya kuidhinishwa ndipo mradi utaweza kuendelea. Hatua zote za usimamizi zilizobainishwa ndani ya ripoti ni lazima zitekelezwe.

